**TAMKO LA MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (MB), WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA DUNIANI TAREHE 9 OKTOBA, 2025**



*Kaulimbiu: "Posta kwa ajili ya Watu: Huduma za Kizawa. Ufikaji Kimataifa"*

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninaungana na jumuiya ya Kimataifa kuadhimisha Siku ya Posta Duniani kwa mwaka 2025**,** siku ambayo inaadhimisha kumbukumbu ya kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Duniani (Universal Postal Union – UPU) mwaka 1874.

Mwaka huu, Umoja wa Posta Duniani unatimiza miaka 151 ya kuunganisha mataifa kupitia mawasiliano na ushirikiano**,** jambo linalotukumbusha umuhimu wa huduma za posta katika kuunganisha familia, kuimarisha jamii**,** na kuziunganisha nchi mbalimbali duniani.

Kaulimbiu ya mwaka huu, isemayo *"Posta kwa Ajili ya Watu: Huduma za Kizawa. Ufikaji Kimataifa,"* inaakisi Dira ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Inatukumbusha kuwa huduma za posta siyo tu njia ya mawasiliano, usambazaji wa bidhaa na huduma za kifedha nchini, bali pia ni kiunganishi muhimu kati ya wananchi au wafanyabiashara na huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi duniani.

Katika Mkutano Mkuu wa 28 wa UPU uliofanyika hivi karibuni jijini Dubai, nchi wanachama zilipitisha Mkakati wa Posta Duniani kwa kipindi cha miaka minne (2026–2029) ukiwa na mwelekeo wa kufanya mageuzi ya Sekta ya Posta duniani. Mkakati huu unalenga katika ubora wa huduma, mageuzi ya kidijitali, ushirikishwaji wa wadau na maendeleo endelevu yanayoendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050**.** Kwa kuzingatia Dira hii, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kufanya mageuzi katika Sekta ya Posta ili kuongeza ufanisi, kuibua fursa, kuwezesha wananchi na kuhakikisha kila Mtanzania ananufaika na huduma zinazotolewa na Sekta hii ndani na nje ya nchi.

Kwa kuzingatia hayo, Wizara ninayoiongoza inakamilisha mapitio Sera ya Taifa ya Posta ya mwaka 2003. Kazi hii ni hatua muhimu katika kuboresha Sekta ya Posta nchini. Sera inayorekebishwa imejikita katika matumizi ya teknolojia za kidijitali, miundombinu ya kisasa na ubunifu katika utoaji huduma; Ushirikishwaji wa Sekta binafsi ili kuongeza ufanisi, ushindani na ubunifu katika utoaji wa huduma; kuwezesha biashara mtandao ili kusaidia wafanyabiashara wadogo na kuongeza kasi ya utoaji huduma; kuimarisha biashara za kuvuka mipaka na kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano ya Posta Kikanda na Kimataifa. Ni imani yetu kuwa Sera mpya ya Posta itawawezesha wananchi, itasaidia biashara, na itaimarisha nafasi ya Tanzania katika mtandao wa Posta wa dunia.

Mageuzi yanayofanyika yanazingatia upatikanaji, ujumuishi, na uendelevu wa huduma. Lengo likiwa ni kuhakikisha huduma za posta zinaendelea kuwa nafuu, bora na zinazopatikana kwa wananchi wote hata wale walio katika maeneo ya vijijini au yasiyo na mvuto kibiashara. Kwa kufanya haya, Sekta ya Posta nchini itabaki kuwa muhimu sio tu katika kuhudumia jamii lakini pia itakuwa kichocheo katika kukuza uchumi, kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na kushindana Kimataifa.

Sambamba na mageuzi yanayofanyika katika Sekta ya Posta nchini, tutaendelea kutekeleza wajibu wa kutoa huduma za msingi za posta kwa wote kwa kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za msingi za posta zilizo nafuu, za kuaminika, na jumuishi. Aidha, Sekta ya Posta pia ina

jukumu la kulinda na kuhifadhi mazingira. Tunahimiza matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira, vifungashio vinavyoweza kurejelewa, na matumizi ya mifumo ya kidijitali ili Sekta ya Posta iendelee kutoa huduma zinazojali wananchi na mazingira.

Tunapoadhimisha Siku ya Posta Duniani kwa mwaka 2025 yenye kaulimbiu *"Posta kwa Ajili ya Watu: Huduma za Kizawa. Ufikaji Kimataifa,"* Tanzania inasisitiza dhamira yake ya kuifanya Sekta ya Posta kuendelea kutoa huduma zinazopatikana kwa watu wote; zinazokidhi matakwa ya wateja na kuimarisha ushirikiano Kikanda na Kimataifa.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea kuunga mkono kikamilifu Sera na Mikakati yote itakayowezesha Sekta ya Posta kuwa nguzo na chachu katika kukuza uchumi, kuleta maendeleo jumuishi na kuimarisha ushirikiano Kikanda na Kimataifa.

*Ninawatakia maadhimisho yenye tija na mafanikio*

*Asanteni sana*